Powered By: manyamfranchise.com

WILAYA YA GATUNDU

MUHULA WA PILI - 2014

DARASA LA TANO - KISWAHILI

MUDA : SAA 1 DAK 40

Soma kifungu kifuatacho kisha ujaze nafasi wazi kutoka 1 -15

Kanini alikuwa ameingojea siku hiyo kwa hamu na ___1___. Wanafunzi __2__ walikuwa likizoni __3__ ya shule kufungwa. Baba __4__ alikuwa amemwahidi kumpeleka katika __5__ ya wanyamapori __6__ mtihani wake. __7__ basi, Kanini alifanya kazi __8__ zote kwa haraka ingawa haraka haina baraka. Baada ya kupata __9__ alichukua __10__ wake na kuandamana na wazazi __11__. Walipofika katika kituo __12__ basi, waliabiri gari __13__ lilikuwa likiondoka wakati __14__. Barasteni Kanini aliona vitu __15__ ambavyo hakuvijua ila alisikia watu wakivisema.

	A	B	C	D
1.	tamu	hamu	ghamu	gamu
2.	wote	sote	zote	yote
3.	kabla	baada	badala	nyuma
4.	yake	wake	zake	lake
5.	shamba	msitu	zizi	mbuga
6.	Akifeli	akipasi	akicheka	akifunga
7.	Hivyo	Hicho	Hil;o	hapo
8.	yake	zake	yetu	lake
9.	chajio	staftahi	chamcha	kisubiri
10.	kikombe	kitabu	simu	mkoba
11.	aliyemsubiri	waliomsubiri	tuliowasubiri	mliowasubiri
12.	ya	la	vya	cha
13.	ambayo	ambalo	ambaye	ambacho
14.	Huo	Hiyo	Hivyo	Hao
15.	mingi	nyingi	vingi	mengi

Chagua jibu sahihi kulingana na maagizo

16. Mmea unaozaa maua yanayotengeneza dawa ya kuwafukuza mbu huitwa __
    A. mbuni
    B. muwa
    C. mpareto
    D. mzabibu

Tumia kiulizi cha idadi (- ngapi)

17. Ng'ombe _____ walichinjwa
    A. ngapi
    B. wangapi
    C. mingapi
    D. zingapi

18. Mpishi ameingia jikono ___ mboga
    A. kukaranga
    B. kukaanga
    C. kuoka
    D. kukarangia

19. $^{3}/_{9}$ huitwa ____
    A. Tatu juu ya sita
    B. tusui tatu
    C. thuluthi tisa
    D. sudusi tatu

20. Chagua kihusishi kinachofaa

Kamau alipiga nguo pasi _____ kuivaa

A. baada ya B. kabla ya

C. kati ya D. mbele ya

21. Chema chajiuza kibaya _____

A. chaanguka

B. chanunuliwa

C. ni mbivu

D. chajitembeza

22. Kanga ni nguo, kanga pia ni _____

A. ndege B. mnyama

C. kupika D. samaki

23. Kanusha sentensi hii:

Waliimba wimbo mzuri

A. hakuimba wimbo mzuri

B. hawakuimba wimbo mzuri

C. waliimba wimbo mzuri

D. usiimbe wimbo mzuri

Andika tarakimu hii kwa nambari

24. Elfu kumi na mbili

A. 1020 B. 12000

C. 1200 D. 1002

Andika wingi wa sentensi hii

25. Mwanafunzi anasoma kitabu

A. Mwanafunzi anasoma vitabu

B. wanafunzi wanasoma vijitabu

C. wanafuzi wanasoma vitabu

D. wanafunzi tunasoma vitabu

Jaza mwanya kwa neno sahihi

26. Kijana ___ atapata zawadi

A. mhondari

B. msafi

C. tukutu

D. hodari

27. Ninayemwita nyanya ataniita _____

A. mtoto

B. mwana

C. kitukuu

D. mjukuu

28. Jibu la alamsikini _____

A. ahsante B. binuru

C. nimeshapoa D. marahabaa

29. Kiungo cha mwili kinachosaidia kupumua ni

A. figo B. mapafu

C. moyo D. ini

30. Chagua kivumilishi kinachofaa.

Wavuvi ____ wanavua ziwani.

A. wasita

B. wanane

C. wasaba

D. tano

Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu swali la 31- 40

Mfalme chuma alikuwa na mabinti wanne ambao walifanana kama shillingi kwa ya pili. Kila adinasi alitaka kumwoa mmoja wao, lakini alitakikana alijue jina la banati huyo. Majina ya mabinti hao yaliwekwa siri kama kaburi.

Nyani alipowaambia wanyama wenzake kuwa alitaka kuasi ukapera na mmoja wa mabinti wa mfalme, walimcheka, wakisema, "wana wa wafalme? Walishindwa kuwapata , wewe utawezaje?"

"Nina hakika nitafaulu," Nyani alisema na kujikunakuna kidevu.

"Mabinti hao wakiziona sura zako mbaya watatapika," Sungura alimwambia Nyani na kucheka kwa dharau. Lakini Nyani hakuacha mpango wake.

Baada ya upelelezi uliomchukua siku nyingi nyani alitambua kuwa kila Jumapili saa nane, mabinti wa mfalme walikwenda mtoni kuogelea. Alichukua kipande cha dhahabu na

kukiweka katikati baraste waliyopitia mabinti hao. Kisha akajificha kando ya barabara. Hakungojea sana.

Saa tano kamili, mabinti hao walipita pale Nyani alipokuwa ameiweka dhahabu.

"Chuchu, tazama dhahabu yangu," mmoja wao alimwambia mwenzake. Kusikia jina "Chuchu" limetajwa, Nyani alikwenda mpaka kwa mfalme na akaozwa Chuchu. Mfalme alikasirika kuona kuwa bintiye aliolewa na Nyani badala ya kuolewa na ghulamu mzuri. Alijuta sana

31. Aliyetaka kuwaoa mabinti wa mfalme ilikuwa ni lazima ajue ___
    A. majina ya mabinti wote
    B. pale mabinti hao walipogelea
    C. jina la baba yao mabinti
    D. Jina la binti aliyetaka kumwoa
32. Mfalme alikuwa na mabinti _____
    A. watatu
    B. wanne
    C. wanane
    D. watano
33. Upelelezi wa nyani ulichukua
    A. miaka mingi
    B. miezi mingi
    C. siku nyingi
    D. siku mbili
34. Mabinti wa mfalme walikwenda kuogelea mtoni ____
    A. kila siku
    B. kila jumapili
    C. kila ijumaa
    D. kila Jumamosi
35. Wana wa wafalme _____
    A. walifaulu kuwaoa mabinti wa mfalme
    B. waliogopa kuwaoa mabinti wa mfalme
    C. hawakutaka kuwaoa mabinti wa mfalme
    D. walishindwa kuwaoa mabinti wa mfalme
36. Sungura alifanyaje ili ajue majina ya mabinti?
    A. Alimuliza mfalme
    B. alifanya upelelezi
    C. aliambiwa na mabinti wenzake
    D. hakujua jina la binti hata mmoja
37. Nyani aliposema alitaka kumuoa mmoja wa mabinti wa mfalme, wenzake __
    A. walimcheka
    B. walikasirika
    C. walifurahi
    D. walimfukuza
38. Nyani alimuoa binti aliyeitwa
    A. binti mfalme
    B. Nyani
    C. Dhahabu
    D. Chuchu
39. Kwa nini mfalme hakufurahi bintiye alipoolewa na nyani?
    A. Nyani hakuwa na mali
    B. Nyani alikuwa na sura mbaya
    C. Alikuwa amemwahidi mvulana mzuri
    D. hakutaka bintiye aolewe
40. Kichwa kinachofaa hadithi hii ni _____
    A. mfalme audhika
    B. Nikahi ya kufana
    C. Bintiye mfalme
    D. Majina ya mabinti yajulikana

<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 -50</u>

Kulingana na uchunguzi wa gazeti moja vijana wengi wanatoroka vijijini kukimbilia mijini. Bila elimu wala ujuzi wowote, wao huishia kuwa wezi, wanyang'anyi na watumiaji sugu wa dawa za kulevya. Dawa hizi ni kama bangi, heroin, miraa na marijuana. Cha kuhusunisha ni kwamba wao huwa na umri mdogo na miaka yao haiwaruhusu kuajiriwa.

Baadhi yao hutoroka shule na kuhamia mjini kwa sababu ya tamaa ya pesa. Wao husahau kuwa elimu ni mwangaza maishani. Sababu nyingine ni kuwa wengi huwa hawataki kujihusisha na kazi za mashambani ambazo wanadai ni ngumu na chafu. Jambo wasilolifahamu ni kuwa maisha mijini ni ghali sana kuliko ya mashambani.

Vijana wanapaswa kutafuta ushauri wa wale wamekula chumvi nyingi. Wasiwe wanawadharau kwani waliliona jua mbele yao. Wakumbuke kuwa kila mzazi hutakia mwanawe maisha bora ya usoni. Wakumbuke pia asiyesikia la mkuu .....

41. Uchunguzi ulifanywa na ____
    A. radio
    B. gazeti
    C. runinga
    D. vijana
42. Si kweli kusema ____
    A. vijana hukimbilia mijini
    B. vijana huwa hawana elimu
    C. vijana hukimbilia vijijini
    D. Vijana hutumia dawa za kulevya
43. Ni ipi siyo baadhi ya dawa za kulevya?
    A. marijuana
    B. kocaini
    C. bangi
    D. chai
44. Vijana hao hawaruhusiwi kuajiriwa kwa sababu ya
    A. utumiaji wa mihadarati
    B. umri wao
    C. kutoroka vijijini
    D. kutoroka mijini
45. Sababu kubwa ya vijana kutoroka vijijini ni
    A. tamaa ya kazi
    B. tamaa ya safari
    C. tamaa ya pesa
    D. tamaa ya safari
46. Kulingana na mwandishi wa taarifa hii elimu ni ___ maishani
    A. bora
    B. nguvu
    C. zawadi
    D. mwangaza
47. Kinyume cha ghali ni _____
    A. ngumu
    B. laini
    C. rahisi
    D. nyororo
48. Waliokula chumvi nyingi ni ____
    A. wazee
    B. vijana
    C. mwandishi
    D. wazazi
49. Waliliona jua mbele inamaanisha
    A. kuona jua mbele
    B. kuzaliwa mbele
    C. kufa kwanza
    D. kutazama jua
50. Asiyesikia la mkuu _____
    A. hufunzwa na mamaye
    B. hufuata upepo
    C. haambiwi tazama
    D. huvunjika guu